

Somo la 5: Manabii wa Mungu

A. Ufunuo wa jumla na maalumu

1. Ufunuo wa jumla ni nini? Zaburi 19:1, Warumi 1:20
2. Simulia wakati ambapo ulihisi uwepo wa Mungu Muumba wetu ulipokuwa ukitumia muda katika mazingira ya asili.
3. Je, inawezekana kwa mtu kumfikia Mungu na kuokolewa tu kupitia ufunuo wa jumla, bila kupokea ufunuo wowote maalumu kupitia manabii wa Mungu? (Warumi 2:14-16)
4. Mwandishi wa Kitabu cha Waebrania anakielezeaje ufunuo maalumu? (Waebrania 1:3)
5. Ikiwa tunaweza kumjua Mungu kupitia ufunuo wa jumla, kwa nini Mungu pia hutoa ufunuo maalumu kuhusu tabia Yake ya upendo na mpango Wake kwa maisha yetu? (Zaburi 119: 105)

B. Jinsi ufunuo maalumu unavyofanya kazi

1. Mtume Yohana alielezeaje mchakato wa ufunuo maalumu aliopokea kwenye Kisiwa cha Patmo? Ufunuo 1:1-2, 10-13
2. BWANA aliwapa ushuhuda gani Haruni na Miriamu kuhusu mchakato wa ufunuo maalumu? Hesabu 12:6-8a
3. Mbali na maono na ndoto, ni njia gani nyingine ambazo Mungu alitoa ufunuo maalumu kwa familia ya wanadamu? Kutoka 3:1-6, Luka 1:26-28, Yohana 1:14-18, n.k.
4. Kwa nini Mungu aliwahimiza manabii wake waandike mafunuo maalumu waliyopokea? (Ufunuo 1:19, Yohana 20:30-31, 1 Wakorintho 10:11, n.k.)
5. Akiwa ameongozwa na Roho Mtakatifu, ni madai gani ya ujasiri ambayo Mtume Paulo alitoa kuhusu Maandiko? 2 Timotheo 3:14-17
6. Ni jinsi gani nabii Musa aliweza kuandika simulizi sahihi la uumbaji, tukio lililotokea maelfu ya miaka kabla ya kuzaliwa kwake? (2 Petro 1: 19)
7. Waandishi wa Injili waliwezaje kuandika masimulizi sahihi ya maisha na mafundisho ya Yesu miongo kadhaa baada ya matukio hayo kutokea? 1 Yohana 1:1-3, Luka 1:1-3

C. Zawadi ya thamani ya Maandiko Matakatiifu

1. Mtunga-zaburi Daudi alielezeaje zawadi ya thamani ya Maandiko Matakatiifu? Zaburi 7:10
2. Nabii Yereimia alielezeaje zawadi ya thamani ya Maandiko Matakatiifu? Yereimia 15:16
3. Ni wakati gani ulianza kuthamini zawadi ya thamani ya Biblia kama ufunuo wa pekee kutoka kwa Mungu?
4. Ni sehemu gani ya Maandiko Matakatiifu unayoona kuwa na maana ya pekee?